



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA MAKAMU WA RAIS**



**BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA  
MAZINGIRA (NEMC)**

**MKUTANO WA WADAU JUU YA UDHIBITI WA KELELE NA MITETEMO  
UTAKAOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA  
JULIUS NYERERE (JNICC) TAREHE 17 MEI, 2023 SAA 3:00 KAMILI  
ASUBUHI**

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) wameandaa Mkutano juu ya Udhhibiti wa Kelele na Mitetemo kwa Wamiliki wa Baa, Kumbi za Sherehe na Burudani / Starehe, Bendi, Wasanii, Wakuzaji wa Sanaa (Promoters), Waendesha Vyombo vya Muziki (DJs), Waongoza Sherehe (MCs) na wadau wengine wa muziki utakaofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) tarehe 17 Mei, 2023.

Lengo la Mkutano huo ni kukuza uelewa juu ya matakwa ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Viwango vya Udhhibiti wa Kelele na Mitetemo) za mwaka 2015. Mgeni rasmi katika Mkutano huo ni Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, CPA Amosi G. Makalla.

Hivyo, wadau wote mnaalikwa kushiriki Mkutano huu muhimu utakaotoa fursa ya kuainisha changamoto mbalimbali na kutoa maoni juu ya namna bora ya kuimarisha Uzingatiaji wa Kanuni na Viwango vya Kelele na Mitetemo bila kuathiri Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za viwango vya Kelele na Mitetemo pamoja na uendeshaji bora wa shughuli za Sanaa Nchini.

*Imetolewa na Mkurugenzi Mkuu  
Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira  
14 Mei, 2023*